

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MJI IFAKARA

TANGAZO KWA UMMA JUU YA UUZAJI VIWANJA ENEO LA KAPOLO (NAKAFURU)

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI WA IFAKARA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA, ANATARAJIA KUUZA VIWANJA VILIVYOPO ENEO LA KAPOLO (NAKAFURU) UMBALI WA KILOMITA 1.5 KUTOKA MAKAO MAUU YA HALMASHAURI YA MJI NA KILOMITA 1.5 KUTOKA BARABARA KUU YA IFAKARA MOROGORO. PIA ENEO LA MRADI LINAZUNGUKWA NA HUDUMA ZA MSINGI KAMA VILE BARABARA, UMEME, SHULE YA SEKONDARI KIBAONI, SHULE YA MSINGI KAPOLO NA MILOLA.

WANANCHI WOTE MNAKARIBISHWA KUCHUKUA FOMU ZA MAOMBI YA VIWANJA AMBAZO ZITATOLEWA KATIKA OFISI YA MKURUGENZI WA MJI KUANZIA TAREHE **16/06/2020 KUANZIA SAA 2.00 ASUBUHI** HADI TAREHE **22/06/2020 SAA 9.30 ALASIRI** KWA GHARAMA YA SHILINGI **20,000/-** TU AMBAYO HAITARUDISHWA

VIWANJA VITAUZWA KWA BEI ZIFUATAZO

- MAKAZI **TSH. 3,500** KWA MITA MOJA YA MRABA.
- MAKAZI & BIASHARA **TSH. 3,700/-** KWA MITA MOJA YA MRABA.
- HUDUMA ZA JAMII **TSH. 3,000/-** KWA MITA MOJA YA MRABA.

VIWANJA VYA MAKAZI, MAKAZI/BIASHARA VINA UKUBWA WA KUANZIA MITA ZA MRABA **491 HADI 789**

VIWANJA VYA HUDUMA ZA JAMII/TAASISI VINA UKUBWA WA KUANZIA MITA ZA MRABA **2503 HADI 3003**

MWOMBAJI ATALAZIMIKA KUAINISHA UKUBWA NA MATUMIZI YA KIWANJA ANACHOHITAJI.

AIDHA, MWOMBAJI ATAREJESHA FOMU KWA KIPINDI KISICHOZIDI SIKU **7** KUANZIA TAREHE YA FOMU KUTOLEWA.

WAOMBAJI WATAKAO KIDHI VIGEZO WATAPEWA TAARIFA NA UTARATIBU WA KULIPIA VIWANJA VYAO PAMOJA NA GHARAMA ZA KUMILIKISHWA.

LIMETOLEWA NA:


FRANCIS NDULANE
MKURUGENZI WA MJI

KWA MAWASILIANO ZAIDI: 0767959142/067833900/0686312447

